# SERA
# YA
# WATAKATIFU

Na

Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad wa Qadian
Masihi Mau'udi na Imam Mahdi[as]

ISLAM INTERNATIONAL PUBLICATIONS LTD

# Sera ya Watakatifu

Tafsiri ya Kiswahili ya: Siiratul Abdaal (Kiarabu)

Siiratul Abdaal (Swahili Translation)

**Mwandishi:**
Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad[as] wa Qadian

**Mfasiri:**
Jamil R. Rafiq

Chapa ya Kwanza (Kiarabu): 1903
Chapa ya Kwanza (Kiswahili): 2021

**© Islam International Publications Ltd.**

**Kwa Maelezo Zaidi:**

**Tanzania:**
Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya, Tanzania
Mtaa wa Bibi Titi Mohamed S.L.P. 376, Dar es Salaam.
Simu: +255222110473 Fax: +255222121744

**Kenya:**
E.A. Ahmadiyya Muslim Mission
P.O. Box 40554 Nairobi Kenya Simu: +254222111031

Kimechapwa na Ahmadiyya Printing Press
Dar es Salaam, Tanzania / Nairobi, Kenya

Cover design: Muhammad Tahir Nadeem

**ISBN:** 978-1-84880-519-4
10 9 8 7 6 5 4 3 2 1

هذه رسالة مباركة ألهمتها بتوفيق الله ذي الجلال وكتبت فيها علامات عباد الرحمن

وما يعرفون به من العلم والكمال الذين يجهل مقامهم وشأنهم كل من هو في سجن الضلال وسمّيتها

# سيرة الابدال

طبعت في مطبع ضياء الاسلام قاديان باهتمام الحكيم فضل الدين بهيروي مالك المطبع في

شهر رمضان المبارك ۱۳۲۱ھ وشهر دسمبر سنة ۱۹۰۳ء من وفات عيسى عليه السلام

تعداد جلد ۷۰۰

قیمت ۱/ر

Jalada la chapa ya kwanza

Hiki ni kijitabu nilichotunga kwa kujaaliwa na Mungu Jalia nami nimeandika humu alama za waja wa Rahmani na ile elimu waijuayo na ukamilifu, ambao daraja yao na shani yao hawaijui wote waliomo ndani ya gereza la upotevu. Nami nimekiita:

# Siiratul- Abdaal

Kimepigwa chapa katika Matbaa ya Dhiya-ul-Islam Qadian, chini ya usimamizi wa Hakiim Fadhl-ud-Diin wa Bhera, mmliki wa matbaa, ndani ya mwezi mtukufu wa Ramadhani 1321 Hijri, mwezi Desemba 1903.

Idadi: 400 bei: Anna moja na nusu.

## Neno la Mwenezi

Kitabu hiki ni tafsiri ya Siiratul Abdaal kilichoandikwa kwa Kiarabu na Hadhrat Masihi Mau‘udi[as], Mwanzilishi wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya.

Abdaal ni istilahi ya dini, maana yake Watakatifu, Mawalii, Masufii na Watawa.

Ndani ya kitabu hiki, Seyidna Ahmad[as] ameandika kwa utondoti sifa bainishi zote, huluka bora na ukweli wa watumwao na Mungu Mwenye enzi. Na sifa zote hizo zimo ndani ya Hadhrat Ahmad[as].

Ufasaha wa matini ya Kiarabu ni kazi bora sana ya ajabu isiyo na kifani. Kimepata kutolewa tafsiri yake kwa Kiurdu miaka michache iliyopita; na sasa kwa kujaaliwa na Mola Mweza nimefasiri kwa Kiswahili. Ingawaje niliweka mbele yangu matini ya Kiarabu pia, lakini nilitafsiri kwa Kiswahili kutoka tafsiri yake ya Kiurdu, iliyo tafsiri safi fika. Hii ndiyo zawadi nyingine ya Dawati la Kiswahili kwa wasemao Kiswahili ili wanufaike nayo kiruhania.

Sheikh Ansar Hussain amepanga herufi zake kwa kompyuta na kutayarisha fomati. Mwenyezi Mungu Ambariki kila aliyeshughulikia kazi hii.

Jamil R. Rafiq
Wakilut-Tasnif
Tahrike Jadid
Rabwah, Pakistan 17 Aprili 2021

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ[1]

نَحْمَدُهٗ وَنُصَلِّيْ عَلٰى رَسُوْلِهِ الْكَرِيْمِ[2]

Enyi watu! Nawatoleeni nasaha ile ile niliyofunuliwa na Mola wa Walimwengu. Nimeagizwa na Rahmani, hivyo nijieni nyote pamwe na ahali zenu. Nimejaaliwa hekima toka mbinguni, sio dhahabu wala fedha. Malaika waliteremka kwa ajili yangu toka mbinguni mpaka ardhini, na Qadian ikafanywa kama ardhi takatifu na mji wa amani. Na Mola wangu Alinihifadhi na shari ya waovu na akanifanya mwenye daraja ya juu. Nikawa na uhusiano kamili Naye. Na kwa ajili ya Rafiki yangu Mpendwa, nyama yangu ya viungu vyangu imeyeyuka, hivyo simwogopi sasa mwenye kuchomoa upanga wala adui mwenye nguvu. Kwani Mola wangu Amesimama kunitetea. Nami naufuata wahyi Wake kwa busara kamili, na jambo langu si la kunitia mashaka wala mie simtungii Mungu uongo. Aipingaye haki simsikilizi, wala sioni uso wa mtu kama mchoyo. Simjali yeyote katika maadui hata kama atishe kunihilikisha; simkabili kama mahawafu. Kwangu mimi, dunia ndiyo kama mwanamke asiye na uso, aliyezeeka, tena anamwasi mumewe, na mume wake anamchukia na anaukirihi

[1] Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

[2] Twamhimidia Yeye na kumsalia Mtume Wake mhashamu.

mwendo wake wa maringo na mapambo yake na kumfahamu kuwa dhalili na mwenzi mbovu fika.

Na afunguaye Sura An-Nuur na Al-Faatiha na Al-Maaida na kusoma kwa makini na kutafakari kama watafutaji wa haki, na ahame kutoka maji kidogo kwenye maji yenye uketo, na kulainisha ufahamu wake na kukata dhati yake vipande vipande; na ajitenge na maji kidogo, asitosheke na bwawa la maji kidogo; asifadhaike na ugumu wa ardhi, wala asichoke kutafuta maji baridi yapitayo; basi mtu kama huyo atapata kushuhudia ukweli wa madai yangu na atakuwa na rai ile iliyo rai yangu na atakuwa miongoni mwa wenye kupata yakini. Kwa yakini kabisa mimi ndimi Masihi Mau'udi, nami ndimi niliyetakiwa kuhilikisha na kufanya ukarimu. Mimi ni mtu nimtafutaye mchamungu anayetafuta haki. Basi, ni habari njema kwa wachamungu. Kwa yakini takwa si kitu rahisi; kwa haki ya Mungu, takwa hushabihiana na mauti, kwani aliyetanguliza takwa ndiye 'mume wa dada ya mkewe' aliyetanguliza mauti. Enyi vijana! Takwa ni kilele ambacho mtu hukifikia kwa mbinde. Hii ndiyo mauti yauguzayo kwa mioto [ya namna namna]. Isitoshe, hii ni farasi bora afikishaye Peponi. Wajuaje kuna masafa kiasi gani baina yake na mauti ya mtu. Ufikiapo hadi

yake ya mwisho na kuikamilisha, basi kwa wenye utambuzi wa Mungu hiyo ndiyo mauti. Kwa yakini mchamungu haziogopi zahama za kishetani, na anafurahia kumwaga damu yake katika njia ya Mweyezi Mungu, kama ndicho kileo kilichochanganyika na maji safi baridi. Na wachamungu wanazo alama ambazo hujulikana kwazo. Enyi vijana! Mchamungu ndiye huwa walii, na katika wakati wa ufisadi wa shetani, hutumwa jumuiya moja miongoni mwa wachamungu kuwarekebisha watu.

Miongoni mwa alama zao, mojawapo ndiyo kwamba wanatumwa katika wakati wa kiza kinachoenea zama zote, nao hudhihirika wapunguapo waungwana na sifa za uungwana, na katika zama hizo watu wenye sifa za nguruwe na wanyama hukithiri; wapendao kuundama huwa wengi; na wasalio tahajudi hupungua; na watu huwa hawafai kitu, hawana elimu wala amali. Zama zinapovurugika vuruvuru na kuwatilifikisha watu wakamilifu, na kuzalisha watoto wenye maradhi ya nyongea [yaani wasio na ruhania]; jicho la mbingu hukauka, halitiririshi machozi; ardhi inakuwa kame, haioteshi mimea; na watu huwa kama mtu aliye na ngamia mwenye nguvu lakini hawezi kumpanda; anao wanja asiotia machoni; na watu wanaipa kisogo haki,

na bonde linafurika tele [na maasi]; basi pamoja na ukame huja hawa watakatifu na kuiondolea mbali hali mbaya, na kuchoma mshale tumboni mwa shetani; na kile kilichoishapasuka hukitililia na kuzing'arisha zama.

Na miongoni mwa alama zao ni kwamba hao ndio watu wasiofadhaika moyoni na heshima ya mtu yeyote, na yule asiyeinama na kunywa katika chemchem ya baraka zao hata sawa na gao moja, hao hawamfahamu hata sawa na kidudu. Nao wanazama ndani ya Uungu wa Mola wao na kumtanguliza katika kila amali na desturi zao. Humsaidia aliyelemewa na mzigo mzito na kumsimamia kwa uangalifu kwa ajili ya manufaa ya huyo. Hawatetemeki mbele ya watawala. Wanalia katika njia ya Mungu Aliyewatuma wakati wa kutapakaa ufisadi wa zama na tamaa za nafsi. Na juu yake huwahimiza huruma ya mahuluku na amri ya Mungu Mwenye enzi.

Na miongoni mwa alama zao ni kwamba pindi uhusiano wao na Mungu Mkarimu unapolegea, huutilia nguvu mpya na kuuchangamsha kwa kuwafanyia hisani watu, nao huruka juu, wala hawakai baada ya kuruka kiasi kidogo. Hunyweshwa kikombe kisichowafanya kuropoka wala kuumwa kichwa. Huendelea kusema, 'je kuna zaidi' wala hawatosheki. Siri zao kwa sababu ya

kuwa nyepesi sana hazifahamiki, kana kwamba wanasema kwa lugha ya Kiajemi. Hujizuia nafsi zao wasifanye jambo Asilolipenda Mola wao, na huimarika juu ya haki. Hawaongopi hata wakitupwa ndani ya moto, wala hawafichi ukweli hata wakikatwa vipande vipande. Na wanapopata kuudhiwa hawakunji kipaji. Humtegemea Mungu na hawaitii maanani dunia wakiiona ni bure isiyofaa.

Miongoni mwa alama zao ni kwamba kabla ya kuzalika njia za ufanisi wao huhabarishwa, nao wanapata habari njema ya msaada wa Mwenyezi Mungu katika zama za kukata tamaa na kukengeuka kwa watu na kukosekana kwa njia za kawaida za dunia hii hakiri, hata kwamba wapumbavu wanayafanyia dhihaka matabiri hayo kudhihirisha, na wanawafahamu kuwa majuha waropokao wazushao uongo kwa kupata matamanio yao, na hao watu wa dunia wanajaribu kuwatowesha na kuwarusha kama vumbi. Wakati huo amri ya Mungu huteremka kutoka mbinguni, nao wanakalishwa mapajani mwa ukarimu wa Mola Mtukufu; na nyavu walizokuwa wamefuma maadui kwa kiburi na majivuno zinanyambuliwa, na mafuriko ya fitina yanakaushwa na hatimaye wanafaulu wakipata ushindi, heshima na adhama.

Na miongoni mwa alama zao ni kwamba unawaona wanaenda mbio kama ngamia jike aliye mwenye nguvu na madhubuti akimbiaye mbio sana; waama mambo ya dunia, basi hawaonyeshi maelekeo kwayo, na wanayakubali kwa karaha tu. Na kwa kupitia hao, Mwenyezi Mungu Hudhihirisha huluka njema za watu na maovu yanayokuwa kama maradhi yaliyofichika. Wao hushabihiana na mvua inayodhihirisha sifa za ardhi; ardhi nzuri huotesha kwa amri ya Mola wake, na kutoka katika ardhi mbovu hutoka mazao mabovu. Ndivyo Alivyotoa Mwenyezi Mungu mfano wa waaminio na mafasiki.

Na miongoni mwa alama zao ni kwamba utawakuta kama mtu mwanana, Kamanda Mkuu mwenye busara na kama mfanyabishara aliye kiongozi wa msafara na mwongozi wa watu wa zama zake. Nao wanapitisha maisha yao wakilia, na kwa ajili ya Mola wao husimama katika ibada na kusujudu usiku mzima; huepukana na mbwamwitu wa tamaa za nafsi na hushughulikia ibada ya Mola wao hadi kufikiwa na mauti. Na watu waovu wanapowatukana na kuwashambulia kama kelbu na kuwafanya kama ardhi iliyofunikwa na ukungu, utawakuta pia katika hali hii kuwa mwenye subira.

Na katika alama zao ni kwamba wanatumwa katika zama za giza totoro, na katika wakati kama huo matunda hupungua sana, na miti hufanana na kuni kavu; na katika zama ambapo usingizi mzito huwashinda watu, na imani ya watu huwa kama shina tu la mti lisilo na matawi; na katika kipindi ambacho kimewalisha watoto wake ulaji mbovu wala hakikuwatunza watu wake wenye njaa, na ndani ya saa ambapo upotevu umewatatanisha, na mbogo za nafsi wametafuna mimea ya matendo mema. Isitoshe, hao sio wenye huluka mbaya kama watu waovu, bali wanazuia ghaidhi yao na humsamehe yule miongoni mwa majahili aliyewaudhi. Nao huwa mashujaa wasiojitupa mbele ya dhuluma iliyopita mipaka hata kama wapo mikono mitupu ndani ya medani ya mapigano. Wanapofikiwa na wasiwasi wa kishetani huomba ghofira. Hivyo matamanio yashambuliayo kama watu waovu, hupata kushindwa, na utulivu unawashukia, na shetani maluuni hukimbia.

Na miongoni mwa alama zao ni kwamba wanamtambua sana aliye kadhabu, mnafiki waziwazi anayeshabihana na lumbwi. Na utawakuta watu watukufu katika mambo yote wenye rai nzuri na mashujaa kama simba, lakini hawaonyeshi tabia ya kinyama. Utawakuta nyoyo

zao hazihitaji kitu, hata hivyo hujinyenyekeza. Huwa wenye kukimbia mbio katika njia ya Mungu, hawahitaji kuhimizwa. Utawaona machozi yao yatiririka mfululizo pasipo kuzuilika. Hawaelekei kutafuta starehe, wala hawatembei kwa maringo.

Na miongoni mwa alama zao ni kwamba takdiri yawaendea kwa kunyapanyapa. Kama ipo takdiri ya kuwashukia balaa fulani, Mwenyezi Mungu Huwahabarisha kabla haijashuka takdiri hiyo. Mauti yawafikia kwa kukawia, hayaji ghafula kama ajali, kana kwamba Mwenyezi Mungu Anasita kuwafisha, na anasitasita kutwaa nafsi *mutma'inna* – nafsi zilizotulia.

Na miongoni mwa alama zao ni kwamba wanaauniwa wala hawaachwi bila msaada; na baina yao na baina ya Mola wao matamanio yoyote hayaingilii kati, wala hawatupwi pasina muawana. Hawatengani na Muumbaji hata kama wasagwe kama kima. Hawawi kama majahili wenye maringo, bali hujaaliwa elimu na hung'arishwa. Mwenyezi Mungu Anadhihirisha mng'ao wao, na wenyewe hawajionyeshi kwa watu. Hutenda mema wakiyarembesha. Utawaona wanastawi hata kama wajeruhiwe. Usiku na mchana huwatolea ushahidi kwamba wa Mawalii wa Rahman hata kama wajinga wawafikirie kuwa hawamwamini Mungu.

Wafikiwapo na taabu humkimbilia Mungu. Mungu Hawaachi katika hali ya kutotambulika, bali wanajaaliwa umaarufu na adhama. Hutamwona kama fisi, bali waonekana vijana wazuri mashujaa. Hutembea juu ya ardhi kwa unyenyekevu wala hawapepesuki kama waliozeeka.

Na miongoni mwa alama zao ni kwamba kundi moja la wasio na elimu wanawadhania vibaya, nao huthibitika kutakasika na tuhuma hizo mbele ya Mungu. Katika misiba hawasikitiki wala hawahuzuniki. Uhusiano wa karibu huwa baina yao na Manabii; hunywa katika kileo ambacho Manabii walikuwa wanakunywa ndani yake. Na wanapofikiwa na taabu huinuka na kurejea kwa Mungu, na chochote walichokuwa nacho hutoa kwa ajili ya Mungu, wala hawafanyi ubahili. Huepukana na kisima cha kidunia, hawasimami ukingoni mwake wala hawaendi karibu nacho. Nao pasina shaka huwa simba wa Mungu wawekwao ndani ya pango la ghaibu. Hakuna simba yeyote wala kipanga kama hao. Huwashambulia maadui na kuwatilifikisha. Wao huwa matawi ya mti wa mahali patakatifu; atakaye kuwavunja, Mungu Humvunjilia mbali. Wanaowazingira, wenyewe wanalia kwa taabu ya kupumua. Na anawaudhi tu yule mjinga afananaye na mmea unaoota kando kando ya

maji ya mafuriko, kisha huchukuliwa na mkondo wa maji, au aliye habithi kuliko nyoka. Kwa neno zima, hao ndio watu ambao Mwenyezi Mungu Mwenyewe anawapigania vita, na maadui wao hawafaulu hata kama wajijeruhi miguu yao wakienda kasi sana, kwani wameshindana na Yule Ambaye kwake wakosefu hawawezi kufichika.

Na miongoni mwa alama zao ni kwamba wawatilia elimu zao watafutaji wa haki nyoyoni mwao. Na huwalea kama ndege amlishavyo kinda wake. Wanao moyo wa kuwapenda, na wanawahifadhi kwa kuwaepusha na mambo yasiyowafaa. Huawasikiliza malalamiko yao kuwafariji wala hawapurukushi. Hao huwa kama wachungaji; waonapo mbwamwitu, huwaita mbuzi zao. Hawajitegemei, bali wanamtukuza Mungu na kumhimidi. Hawaishi kama wale wapendao starehe, bali wanapofikiwa na huzuni baada ya huzuni hulainika. Na nafsi zao zinatakaswa na Mola wao hata kwamba jazba zao za nafsi hufutika moja baada ya nyingine, hatimaye roho pekee hubaki, nao wanakuwa wa pekee, ndipo wanatumwa kwa watu, nao huwaita kwenye wema na ufaulu. Hii ndiyo daraja ya Ma-Abdaali – watu watakatifu – walioshika njia zile ambazo kwa kuzikanyaga hizo hatimaye hawajuti wala hawasikitiki.

Wanapita katika mabonde wasimoweza kupita watu wazito. Nao hawafi mpaka wanapoacha nyuma yao jumuiya ya watu wanaojaaliwa maarifa, nao huwa wamchao Mungu. Humwita kila mwenye kuangamia asiyejua kwenye chemchem yao wala hawachoki. Basi Asikiaye sauti yao huwajia, lakini wale walio viziwi ambao ndimi zao zimechubuka kwa sababu ya kuugua, na waliopatwa na shtuko la moyo, hao hawaelekei. Na makafiri wamekuwa na desturi ya kutosikiliza sauti ya waliotumwa hata kama waitwe kwa sauti iliyojaa uchungu; hawazinduki kwa sauti ndogo au sauti kali mpaka adhabu huwashika, nao hawatambui. Manabii hujibidiisha asaa Mwenyezi Mungu Akawaondolea ukungu wao na wakaanza kuona. Lakini hukaa tu kama mwanamke aliyetalikiwa, na humwasi Mola wao; na hukengeuka kana kwamba hawajui. Hufyatuka akili kama mtu aropokaye, nao wanakuwa wenye huluka mbaya na wenye midomo michafu, huwatusi Manabii na kukosoa. Wanakula, hawashibi. Wale walioamini wanajitahidi katika njia ya Mungu. Ingawa hukanyaga nyayo zao haraka sana kusonga mbele, hata hivyo wanazilaumu, kwani wanafikiria wanarudi nyuma. Huvumilia taabu kwa ajili ya Mungu ili wapate kukubaliwa. Hivyo, rehema ya Mwenyezi Mungu pia inawasaidia wala hawaachwi ndani ya maisha magumu,

bali hurudi na mafanikio. Mtu duni anawafikiria kama mmea usiofaa unaoota ndani ya shamba la ngano, ilihali mahuluku wapo salama kwa sababu yao. Hao wanatafuta ridhaa ya Mungu na wanapiga kelele kama mwanamke mwenye uchungu wa kuzaa, ndipo wanaingizwa ndani ya wale wanaokubaliwa.

Na Miongoni mwa alama zao ni kwamba Mwenyezi Mungu Anawaondolea ukali wa uchungu na mashaka na kutowesha wasiwasi nyoyoni. Hivyo, kila wakati nyuso zao zinang'ara wala hawatishiki. Hujaaliwa huluka ambazo mfano wake haupatikani katika wengine. Wanatambulika wakati wa kukutana nao. Huwapokea wageni kwa heshima hata kama mmoja wao ni hadimu wa kanisa, au ni mtu asiyestaarabika kama punda wa mwitu; desturi yao ndiyo hii hii.

Na miongoni mwa alama zao ni kwamba hawana njia ila kwa Mungu. Hujitenga na mto wa kulalia. Kwao maji yanukayo ndiyo maji baridi katika njia ya Mungu. Hutaka ridhaa ya Mungu, na dunia machoni mwao ni kinyesi cha mnyama; na aitafutaye dunia ni mtu bure asiyefaa, au ni fisi kama baba ya Ibrahimu. Nao hupewa vishada vilivyo karibu yao na matunda; na kwao dunia ni kitambaa ambacho kwacho Mwenyezi Mungu Anaondoa kwenye jiko chungu cha maisha yao, hivyo hawapati

madhara. Hiyo ni hidaya kutoka kwa Mola wao wanapojitenga na dunia na kuisahau. Basi, humwendea Mungu wanguwangu na machozi yao hutiririka kwa kumkumbuka Yeye. Hao ndio waja wanaoifahamu dunia sawa na kiasi kile anachochukua sisimizi kinywani mwake, ambapo kuishughulikia ni upotevu. Hii ni visu ambavyo huchinjwa navyo, na waitakao dunia ndio wanambuzi. Maji yake ni kidogo na ulaji wake ni hilaki. Tabia yake ni kama ya mwanamke anayeitwa na mumewe lakini anakataa kwa kisingizio cha kuwa mwezini, naye sura yake ni kama ya mwenye kukauka ngozi yake, hakuna uzuri uliobaki ndani yake. Mwanzo wake ni raha lakini mwisho wake ni dhiki. Hutamkuta dhalili kama yeye. Hii ndiyo mpungate, usiidhani kuwa kichala cha zabibu. Ndiyo sababu waja wa Rahmani wameichomolea upanga wa kuikata vipande vipande. Hawakuishika kwa mikono yao, wala hawakutaka kuichuma, nao wameitaliki talaka tatu. Hao sio kama mwanamke mwenye maradhi ya kuharibu mimba. Huwa wakamilifu katika kauli na matendo. Hawajali damu kutapakaa mwilini, kwani huwa tayari kupokea mauti.

Na miongoni mwa alama zao ni kwamba wanakulia kama yule mtoto aliyelishwa mlo bora. Na tabia yao ya kuogelea kwa kasi sana huwa kama samaki wa baharini

aitwaye [kwa Kirabu] ‘ankad. Na baraka zao ni kama za mvua iendeleayo kunyesha. Ukweli unapokuwa kama mti uliong’olewa, ndipo hudhihiri. Na kama zama hazinao hao, basi zama hizo zimekosa mvua. Na fitina na maafa yanapokithiri, basi hayo ndiyo harufu nzuri za kudhihiri kwao na ni dalili ya ujaji wa nuru yao. Hupiga mbio katika njia za Mungu kama farasi akimbiaye mbio sana. Hutambua siri za watu kana kwamba wameishapasua tumbo. Ujaji wao ni ujaji wa mwanga, na kuondoka kwao ni giza. Hao ndio changamsho la dini na ni hoja ya Mungu ardhini. Ujumbe wao huenea kama kimulimuli cha radi na kama bahari ifure na mawimbi. Watu wema huwaendea kama kulungu atokezavyo katika makao yake. Kwa kuwaacha wakaidi, wenye tabia njema wanawakubali. Na wakanushao, hakuna budi watatambua matokeo yake wakati wa gharighari ya mauti, japo leo wanawaka kama moto uwakao. Hao watu wanaitanguliza dunia na kuifanya mahali pa ibada kwa nyoyo zao; huielekea kikamilifu jinsi jimbi amkimbiliavyo koo kwa kupandana akieneza mabawa yake. Hao huwa imara katika ujinga kama kamba iliyosokotwa. Hawawi kama kishada safi, bali ni kama chakula chenye kuvu. Hawana heri yoyote, nao huwa kama bahili. Kwa yakini wanaowaamini mitume wa Mwenyezi Mungu,

mfano wao ni kama mti mzuri uliopo kwenye vilima vya mchanga wenye rutuba; ndio hao wanaofanywa wasaidizi wa dini tukufu. Hupiga mbio katika njia za Mungu, kwani wanafumbuliwa macho yao. Huondolewa joho la kibinadamu na tumba la imani yao [baada ya kuchanua] hutoa matunda. Japo ndio simba, lakini sio wenye huluka mbaya. Na hawawi wazito kwa kutengana na dunia, ndiyo maana hudumu kuruka kumwelekea Mungu, wala hawawi wenye kukimbia kwa miguu mizito. Huufagilia undani wao hata hawaachi kubaki humo chembe moja ya dunia. Amali yoyote waifanyayo, hufanya kwa ajili ya Akhera, na hujitahidi kwayo. Hupewa lulu za maarifa zisizotobolewa, nao hupata maarifa mepesi ya ndani sana mpaka mjinga mwenye kiburi anawadhania kuwa wakana Mungu. Unaziona nyuso zao kama tawi laini jororo; nao kwa sababu ya kumtambua Mola wao hawanao weusi nyusoni mwao, nao hawakati tamaa. Huwa na heshima huko mbinguni, hivyo wanaowavunja heshima, au kumwaga damu yao, Mwenyezi Mungu Hupigana nao vita. Basi wanakamtwa na kung’olewa mbali, hao ndio viziwi, mabubu na vipofu na kwa ukali wa inadi hupata maradhi ya moyo.

Na miongoni mwa alama zao ni kwamba maji ya hodhi yao hayachafuki; hujaaliwa kila wakati maji yapitayo, wasijue maji yenye matope ni kitu gani, hupewa mfululizo maji baridi matamu. Mola wao Anawajaalia mlinzi, hivyo wanakingwa na nyika na mbwamwitu waliopo humo. Na kiriba cha nafsi zao hujazwa nuru na ufahamu; mambo mengi yanayofichikana kwa *mahjuub* – ambao kuna pazia baina yao na Mungu – hubainika kwao.

Hii ndiyo kwa sababu hao – watakatifu – wanajitupa kwa Mungu kama ndama achinjwaye; hao ama wanatimiza nia yao au wanangojea, na pia kwa sababu wanatoa mali yao yote kwa ajili ya Mungu pekee, wala hawawi kama mtu bahili. Hutoa matunda kama kishada kizuri kirefu, hivyo maskini wanakuja katika himaya yao. Hupewa riziki pasipo kutia bidii au kuomba kung'ang'ania kutoka kwa Mungu Awalindaye watu wema.

Na miongoni mwa alama zao ni kwamba Mwenyezi Mungu Anawatilia nafsini mwao kiu kali ya maarifa kamili. Vifua vyao vyapasuliwa na ghasia za kibinadamu hutupiliwa mbali kikamilifu, kisha hujazwa huba ya Mungu. Kwa ajili Yake hujichinja nafsi yao kama ng'ombe. Wanarundika mafao ya takwa na huendelea kutoa wakati wote sawa na haja. Na

huepukana na kila mpumbavu. Na huondoa mabaya kwa njia ya kutenda mema. Hujinyenyekeza kwa ajili ya Mungu, na kuishi kama mtu mwenye nywele timtimu na mwenye mavumbi. 'Huuivisha' ukaribu wao na Mungu jinsi chapati ipikwavyo kwa kuivisha juu ya makaa ya moto. Ingawaje wanao ndugu na watoto wengi, huishi kama mtu asiye na ndugu wala mwana. Nao kwa kutekeleza amri za Mungu Aliye Mmoja, huwa kama ardhi ioteshayo haraka. Hawayajali masuto ya wadhalimu wala kwa tishio hawaendi kombo hata kidogo katika njia walizojichagulia. Hupamba nyumba ya nyoyo zao kama mwanamke stadi. Huinuka kwa ajili ya Mungu kwa sururi, na chochote wanachopata kutoka kwa Mungu hukishika kwa nguvu.

Na miongoni mwa alama zao ni kwamba ukikaa pamoja nao kwa muda fulani, utashuhudia maajabu kutoka kwao, nawe utawakuta kama ngamia jike atoaye maziwa mengi. Maneno yao huzisafisha nyoyo na mazungumzo yao yanapenya mioyoni. Basi huwa wanapambwa kwa umbile asili la takwa kwa amri ya Rahmani, na sehemu iliyozidi ya matamanio ya nafsi hukatwa, na yaliyokwisha kusanyika katika madhambi hufutika. Na ni wengi walioje vipofu wasiojihadhari wanaoanza kuona, na kupitia hao wakistaarabika

wanakuwa watawa na watambuzi wa Mungu. Hivyo, ole wao wanaowafanyia masihara kama yule mwanamke anayebweka mbele ya mumewe; hawaelewi wataangamia tu kwa kutalikiwa, kwani Mwenyezi Mungu Ameambatanisha wokovu wao na huba ya watakatifu na ukarimu wao. Hivyo ameangamia yule mtu aliyetengana nao, kwani akaachana na waliokuwa walinzi wao. Hii bahati mbaya ni ya mtu mwenye uzembe kamili katika tabia yake, na papo kwa papo hufanya papara na majisifu, naye hayuko pamoja na wanaomcha Mungu na wenye kufanya tadbiri. Hayo yote huzalika kwa uchafu wa kidunia. Basi, ole wao wanaojichafua kwa uchafu huo. Hao wakiwafukuza waja wa Mungu na kuwadhihaki, hujaribu kuwaudhi na hufikiria wanatenda tendo jema. Wakati huu madhalimu mkubwa kuliko wote ndiye yule aliyeko tayari kuniudhi na ndiye mfitini na mwenye kiburi aonaye kama shetani kwa hasira. Yeye alinitisha kama chatu kwa mlio wake. Naapa kwa Allah kwamba nimo ndani ya himaya ya Mungu Aliye Rahmani. Hivyo, aliyetaka kunikata, yeye atakatwa kwa mikono ya Mungu Dayani. Mimi nipo mbele ya macho Yake, na mitume hawaogopi mbele ya Yake. Na njama za wenye njama zitarudishwa kwao, laiti wangejua!

Na miongoni mwa alama zao ni kwamba hao hawawi kama mahawafu ndani ya medani ya vita, bali huwa thabiti, wala hawaonyeshi woga; wanawaongoza watu kama mtu mahiri ili waweze kuwahifadhi wamwogopao mbwamwitu. Na wanarudi na maarifa kama ajaye na kitu bora kabisa. Hawaitegemei bidii ya nafsi zao. Na huogopa siku ya kubomoka jengo la umri wao na kuvunjika, hivyo humwomba Mwenyezi Mungu kujaaliwa warithi, nao humkuta warithi kama kijana aliyebalehe. Huvunjilia mbali jazba zao kwa kujipatia ridhaa ya Mola wa walimwengu. Huhalisika kwa Mola wao wala hawachanganyi kitu ndani yake. Hawaachi kizingiti cha Mungu, na huba ya Mungu hupenya nyoyoni mwao, na wanaambatanisha nafsi zao na Mpendwa wao. Hawawakasirikii watu, bali wanahifadhi ndimi zao. Na kama kwa bahati wapate kutamka neno la hasiria, wanalifidia kwa upole. Huongea kama mtu fasihi, na ndani ya maneno yao ufasaha huja kwa fadhili za Mola wao. Huwatolea fukara mali nyingi. Na katika medani za majaribio wanaendelea mbele kama mashujaa kwa kuyakabili. Wakati wa ghaidhi hutawaona uso umewaiva. Katika msiba utawaona wanatazama upande wa Mungu kama samaki wainuao vichwa vyao. Shingoni mwao huwa kamba ya mahaba ya Mungu sio kitanzi

kilichotengenezwa na kano. Anawashambulia yule tu aliye dhalili; na anawaudhi yule aliye mwenye bahati mbaya zaidi kuliko *dayyuuth* – ajuaye kwamba mkewe anazini, lakini hajali. Azma yao huwa imara na yenye nguvu kwamba wakusudiapo jambo fulani hulichukulia hatu kwa nia imara. Na yatokeapo mapigano na nyoka, humkata vipande vipande. Na mtu awafikiaye mara kwa mara akiwa na kiu, yeye anatoshelezwa na huondolewa shaka ya kila namna. Zama za kukata kiu zimewadia, hivyo iwe habari njema kwa wachamungu watafutao haki. Je hamwoni kwamba zama zimeharibika na zimejaa wasiwasi; kuta zake zipo karibu kubomoka. Magonjwa yanatapakaa, na watu wanakufa. Vifo vimezidi kila mahali. Elfu ya sita ya zama imekwishapita, nami nipo kwenye mwanzo wa elfu ya saba. Enyi vijana! Manabii walinena hivyo. Basi mpaka lini mtanikadhibisha, na hamtamwogopa Mola Mwenye kutoa malipo na kuadhibu.

Na miongoni mwa alama zao ni kwamba hutaka Pepo kwa kumlaki Muumbaji Mtukufu sio kwa ajili ya nyama za ndege na zabibu nyeusi. Utakuta shabaha yao ndiyo kuyakimbilia maamrisho ya Mola wa dunia na Akhera wakinyoosha mikono yao. Wakaondoa mapazia ya sheria, na kwa ukweli wao wakaambua ulimwengu wa

kiungu uliokuwa umeambatana ambamo mwenye kwenda kumlaki Mungu anapata daraja ya kujipoteza ndani ya Mungu. Hayo ni kwa sababu Mwenyezi Mungu Aliwaonyesha maonyesho mengi ambayo kwa sababu yake wakabomoa jengo la dhati yao na hazikubakia ndani yao harakati za kinafsi, nao wakaingia ndani ya amani ya Mungu kujilinda na majoka. Wakaingia bustani na nyuso zao zikang'aa kama mng'ao wa umeme. Wakazikuta nyuso za wapendao dunia kuwa nyeusi, na wakajaribu kuzing'arisha. Wakawa tayari kuwarekebisha jinsi kuku anavyoatamia. Humsaidia kila apigaye kelele kuomba msaada hata kama anajisingizia tu, isipokuwa wale anamotaga mayai shetani na kutotoleka humo vifaranga. Hawa ndio waja wa Mungu; anayewakadhibisha ndiye kadhabu mwenyewe, na akapoteza urembo wa takwa na kuinyolea mbali. Wale wanaowafanyia uadui hao watakatifu, hufanana na mwanamke mpujufu; na shambulio la mwanamke mwenye mdomo mchafu na huluka mbovu haliwezi kuwadhuru. Wakati wa kukabiliana, mikono ya maadui hao hupasuka nao huikimbia medani ya vita kama mabweha. Na utayakuta maelezo ya viongozi hao watakatifu kama kinywaji kipitacho kooni kwa urahisi, nayo hupenya nyoyoni na kuziondolea mbali dhambi. Na

Mwenyezi Mungu Anafuta zile tuhuma za uongo wanazonasibishiwa; na Huwafanya kwa marafiki zao na ndugu zao kama ngamia jike ili wafaidike naye. Naye kupitia hao Anawaponya maradhi ya upofu na ugonjwa wa wenye kiburi na wenye kufuata shetani aendaye kisirisiri kwa hila. Mjinga pekee anawafanyia uadui; mchamungu mnyenyekevu tu anawakubali. Makwao yao huharamishwa kwa mafasiki wanaokimbilia maovu kwa kusudi, nao huridhika na kuvumwani na hukaa mbali na maji yapitayo.

Na miongoni mwa alama zao ni kwamba wanachuka kidogo sana katika dunia, na katika dini wanachukua kwa wingi. Hupata katika neema za dunia kadiri anayochukua sisimizi kinywani mwake; lakini huchukua sehemu kubwa katika takwa. Hunyoosha nafsi zao jinsi mtengenezaji wa uta anyooshavyo mshale wake. Hung’olea mbali tamaa za nafsi zao, na hubaki ridhaa ya Mola kama shina jadidi la mti, nao wanakuwa imara juu yake, na kuitanguliza katika kila njia, wala hawajali ghasia za wajinga, wala hawajali kujua hao ni watu gani; na mjeledi wao [wanaopigwa nao] wanauona ni tawi jororo, wala hawatishiki. Na elimu waipatayo, huipata kwa sababu ya mahaba yao, sio kwa kazi ya sulubu. Hunyweshwa kwa ghaibu, nao hunywa mpaka

kutosheka. Hukata uhusiano na wote ghairi ya Mungu kwa mkuki mkali. Nao kwa ajili ya Mungu hujichagulia njia nyembamba, na Iblisi hathubutu kuwatia katika taabu wasimoweza kujitoa, huiondoa kwa nuru zao. Hivyo, kiriba kilichojaa wanachokuwa wamekibeba, shetani hawezi kupunguza humo hata sawa na chembe, naye anaziogopa nyuta zao wanazoziimarisha na kurekebisha kwa kuzitia ndani ya moto. Hutawakuta kuwa wenye maneno mengi makavu, bali utakuta uzuri na maarifa katika usemi wao. Wakapigana vita na matamanio ya nafsi, na wakapigana vizuri mno. Hao ndio wenye lubu na walioongoka. Hunywa yaliyomo ndani ya 'chombo cha kumkurubia Mungu' kwa kupiga mafunda, kwani huwa wamejitupa kwa Mungu Mmoja kama fukara, na kwa sababu hiyo hao ndio kama wenye tamaa katika njia ya kwenda kumlaki Mungu, nao hawatosheki. Hutanguliza kilicho bora na kitamu sana. Na Mwenyezi Mungu Anawaondolea matamanio ya ghairi Yake na kuyakata. Mungu Huwajaalia uwezo wa kutupilia mbali kila kitu ghairi Yake na kuwawezesha kusogelea Kwake kwa njia bora ili kila mwenye hila mbaya atambue kwamba hao ndio wakweli.

Na miongoni mwa sifa bainishi zao ni kwamba wanatakaswa na uchafu wa kibinadamu jinsi mwanamke anavyotakasika na hedhi. Mwenyezi Mungu Anawaelekea kwa rehema, hivyo wanavutika kwake. Hutilifikisha nyumba ya nafsi yao kwa mikono yao na mikono ya Mungu; humwona Mungu kwa macho yao ya kiruhania. Wanatakaswa na kila shaka, na kukamilishwa katika elimu. Kwa Mungu, daraja yao inazidi kuliko malaika, kwani wakajipinga nafsi zao, na wakaimarika kama pande la mtu kwa kubeba mzigo mzito. Moto wa mahaba yao ukawaka na mwiba wao ukatoweka na makali ya panga zao yakanoleka, bali wakapasulia mbali kila pazia na kujipoteza ndani ya huduma ya Mungu Mmoja. Basi haupiti wakati wao wowote ela huwa wanafanya ibada. Na Mwenyezi Mungu Huzizuia nyoyo zao zisielekee kwa ghairi Yake, na Huwatilia hamu ya mapenzi Yake. Hivyo, kila chembe yake huinama kwa Mola wake, na huba ya Mungu huwa mlo wao wanaolishwa. Nao hula haraka sana isije mwingine akaichukua, kwani watu hao huwa wenye ghera. Hulia kwa ajili ya Mpendwa wao mpaka kope zao zinakuwa tupu – hazina nywele tena. Ghamu kwa ajili Yake huunguza moyo wao, nao hujaa kama kiriba kwa kumkumbuka, na wakati wote wanakosa utulivu kwa ajili Yake. Nyoyo zao zinakuwa na harara

kama jiwe la moto kwa mahaba ya Mungu, kwa hiyo kiu yao huzidi. Wanayo daraja kwa Mungu wasiyoijua mahuluku, ndiyo maana watu wanawadharau na kuwatuhumu kwa tuhuma chafu.

Na katika alama zao ni kwamba hawatishiki kwa zahama za fitina, bali huvuka bahari za majaribio jinsi mashua zipitavyo kwa kukata mawimbi. Huwa hawachanganyi haki na batili, na huchukia kitu chenye mashaka. Hupenda ile takwa isiyo na doa, nao wanahalisika kwa ajili yake, hawataki rangi nyingine kuingia. Mvua yaendelea kunyesha sana mfululizo juu ya ardhi yao, na kwayo hustawi. Wanao mkuki unaomuua mbwamwitu. Asili yao tukufu huwa kama kilima kirefu kwenda juu. Chungu cha huba yao ya Mungu huchemka nao wanaiva. Akaaye pamoja nao, hata kama amezama ndani ya mapenzi ya dunia, hata hivyo kwa baraka ya hao wacha Mungu, atapita kutoka katika tundu la sindano; na yule aliye miongoni mwa wamwabuduo shetani, akihudhuria kwao, atakuwa kati ya wale wasiofanya upujufu. Na yule aliye shetani, akiwa mwaminio, awe mwaminifu kwao na ajinyenyekeze mbele ya amri ya Mungu, basi atakuwa miongoni mwa watu walio wachamungu. Ewe msikilizaji! Usistaajabike; shani yao ndiyo kubwa zaidi

kuliko hiyo; nami niielezeje msipoweza kuielewa. Hao ndio watu waliao sana ambao machozi yao yatiririkayo ni mengi zaidi kuliko maji mnayoyanywa.

Na miongoni mwa alama zao ni kwamba katika rundo la amali zilizokafuliwa hutenganisha amali sahihi za kweli, na makununu yanayosalia huwaachia waliopotea. Huchukua kitu halisi, wala hawafuati ubahili. Hushughulikia daima kutafuta haki; na hudumu kukitikisa kila kitu mpaka kidhihirike kilicho chini yake, na kianze kutiririka mbele ya macho yao walichokitafuta. Hawakatai jambo walikataalo majahili, bali huchunguza. Hawaishi kama mafukara duni, bali hukusanya vitu bora sana vya soko la Akhera, wala hawaghafiliki. Sauti ya kiherehere cha moyo wao ni kama sauti ya chungu kilichochemka, na kwa gongo hili wanamchapa Iblisi. Hujiepusha na kila ufisadi kwa ajili ya Mpendwa wanayemtanguliza juu ya kila kitu. Wakavunja magego ya nyoka aliyemdanganya Adamu, nao wakamchapa yule nyoka kwa mjeledi wenye kujeruhi, hivyo haiwezekani kwake kuwashambulia, bali akawakimbia watu wampigao mawe. Wakawashambulia kama simba, nao wakajilazimisha nafsi zao kuung'olea mbali mzizi wake na kuwaokoa katika shari yake, na kuwaachisha. Nao hukata nywele zake jinsi manyoya ya

mwanakondoo yakatwavyo, ili aonekane rabana. Na humjeruhi kwa mikuki. Shingo zao huinama kwa Mola wao, nao wanakuwa watiifu wake tu. Hao ndio watu ambao kwa sababu yao jicho la mahuluku limepigwa na butaa; hao wamewashangaza hata malaika pia. Wakajiweka nyama zao ndani ya sinia ya Mungu Mmoja, na Mungu Akala vyote vilivyokuwa kwenye tandiko la chakula; wakaliwa kwa vyanda vya huba; na wakajifia kwa ajili ya Mpendwa Yule waliyemhiari.

**TAMATI**

Mirza Ghulam Ahmad Qadiani
Tarehe 14 Desemba 1903